18. Dada wa mke wako – Shemeji / Kaka humwita mke wangu mwamu.
19. Kaka ya mke wako – Mwamu / mlamu.
20. Dada ya mume wako – Wifi.
21. Baba ya mume wako – Bavyaa.
22. Mama wa mume wako – Mavyaa.
23. Baba ya mke wako – Baba mkwe.
24. Mamaa ya mke wako – Mama mkwe.
25. Wanaume walioоa watoto wa nyumba. moja(dada) huitana – Mwanyumba.
26. Mzazi wa mume na mzazi wa mke huitana – Kivyele.
27. Mke wa mwanao – (Mkaza mwana) / Mke mwana.
28. Mama asiye mama yako halisi – Mama wa kambo.
29. Wake waliolewa kwa mume mmoja huitana – Mkemwenza / Mitara.
30. Mtoto wa shangazi / mjomba / ami / halati - Mkoi / Binamu.
31. Mtoto wa wifi / Mwamu / Shemeji – Mpwa.
32. Mwanamke aliyefiwa na mume – Mfaruku.
33. Mtoto wangu wa kike – Binti / banati.
34. Mtoto wangu wa kiume – Bin.
35. Mtoto wangu wa kike – Binti.
36. Baba wa babu – Babu mkuu.
37. Mama wa nyanya – Nyanya mkuu.
38. Wazazi wa mume au mke – Wakwe / wacheja.
39. Mke wa amu – Mkaza amu.
40. Ndugu anayekufuata nyuma – Ndugu mlungizi / Mnuna

**MAJINA YA WATU MBALIMBALI**

1. Mtu mwenye ujuzi wa kuzalisha – Mkunga.
2. Fundi wa mbao - seremala.
3. Anayetengeneza vyombo vya Udongo – Mfinyanzi.
4. Mtu anayetengeneza vitu vya pete – Sonara.
5. Anayefanya kazi ya kuwasonga watu nywele – Msusi.
6. Anayewakilisha nchi yake katika nchi fulani – Balozi.
7. Anayebeba kazi kwa mkokoteni – Hamali.
8. Anayebeba mizigo akitumia mgongo / kichwa / mkono – Mpagazi.
9. Anayefanya kazi ya kupakua na kupakia mizigo kwenye meli / jahazi – Kuli.
10. Anayefanya kazi ya kunyoa watu nywele – Kinyozi.
11. Anayefanya kazi ya kulinda mlango – Bawabu.
12. Anayeendesha ndege – Rubani.
13. Anayeamua mashtaka kwa mujibu wa sheria za kiislamu – Kadhi
14. Anayezinadi vitu katika mnadani – Dalali.
15. Mwenye elimu ya kiislamu na aghalabu hufundisha watu wengine – Sheikh.
16. Mwenye anawakilisha watu wake katika halmashauri ya mitaa – Diwani.
17. Anayeamua kesi kortini – hakimu.
18. Anayewakilisha watu kesini – wakili.
19. Msichana ambaye amebaleghe lakini hajaolewa – Mwanamwali.
20. Mvulana ambaye amebaleghe – Barobaro.
21. Mwanamke asiyezaa kizazi – Tasa.
22. Mwamamume aliyefika umri wa kuoa lakini hajaoa – kapera.
23. Mwanamume asiyezaa kizazi – Mgumba.
24. Mwanamke / mwanamume aliyefiwa – Mjane.
25. Msichana ambaye hajavunja ungo – Bikira / Batuli.
26. Anayetumwa kupeleka barua – Tarishi / katikiro.
27. Anayepeleka barua za posa – Mshenga.
28. Anayeuza bidha rejareja – Mchuuzi / Bazazi.
29. Anayetahiri vijana ukumbini – Ngariba.
30. Mpelelezi katika nchi ngeni – Jasusi.
31. Anayesaidiana na dereva katika matwana – Utingo.
32. Bingwa wa kutunga nyimbo – Manju.
33. Anayetunga mashairi na kuimba – Malenga
34. Fundi wa kupiga ngoma – Sogora.
35. Fundi wa mashini / mitambo – Mhandisi.
36. Anayelinda farasi / anayepanda farasi – Saisi.
37. Anayejenga nyumba za mawe – Mwashi.
38. Anayewakilisha watu wake katika baraza kuu la taifa – Mbunge.
39. Kiongozi wa wanafunzi shuleni – Kiranja.
40. Kiongozi wa nchi iliyo jamuhuri – Rais.
41. Mfua nguo na mpiga pasi – Dobi.
42. Anayeendesha meli – Nahodha.
43. Anayeendesha gari la moshi – kandawala.
44. Anayeongoza meli bandarini – Serehangi.
45. Anayejipendekeza ili apate kitu fulani – Barakala.
46. Anayetafsiri lugha moja hadi nyingine – Mkalimani.
47. Mtu asiye na mali - maskini / fukara / fakiri / mkata.
48. Anayefunza wasichana mambo ya utu uzima – Kungwi.
49. Anayafundisha wavulana mambo ya utu uzima - nyakanga / somo
50. Anayewinda wanyama mwituni – Mwindaji.
51. Anayewakopesha watu pesa na kuwatosha faida – Mlariba.
52. Mtu apandaye mnazi ili kuangua nazi – Mkwezi.
53. Aliye na utaalamu wa nyota – Mnajimu.
54. Mwanamke anayeshika mimba kwa mara ya kwanza – mwanagenzi.
55. Anayeiba vitu kutoka kwa mifuko ya watu wengine – Mpekuzi / mchopozi.
56. Anayetengeneza vyombo vya chuma – Mhunzi.
57. Anayezaliwa na wazazi wa rangi tofauti – Chotara / shombe / suriama.
58. Asiye na chembe za rangi mwilini – zeruzeru / Albino.
59. Mtu anayependa kula mara kwa mara – Buge.
60. Mchapishaji wa vitabu na gazeti – Mhariri

61. Achotaye maji na kuyauza – Mzegazega.
62. Msimamizi wa kazi - mnyapara.

**Vilema**

1. Asiyesikia - kiziwi
2. Asiyeweza kusema - bubu
3. Asiyeweza kuona - kipofu
4. Asemaye kwa kusitasita - kigugumizi
5. Aliyelemaa miguu - kiwete
6. Anayeongea kwa ncha ya ulimi - kithembe
7. Aliye na nundu mgongoni - kibyongo / kiduva
8. Mtu mfupi kuliko kawaida - mbilikimo
9. Asiye na akili timamu - punguani / wazimu
10. Aliyepindika miguu kwa ndani - mang'ombo
11. Aliye na jicho moja lisiloona - chongo
12. Aliyekatika sikio - kibunye
13. Aliyekatika pua - toinyo
14. Aliye na mboni za macho zilizokwenda upande - kengeza
15. Aliye na sehemu zote za siri - huntha

**VITENDAWILI**

1. Nameza lakini sishibi – Mate.
2. Mlima sipandi – Maji.
3. Ubwabwa wa mwana mtamu – Usingizi.
4. Nyumba yangu ina nguzo moja tu – Uyoga.
5. Kurunzi ya Mola haitumi mawe – Mwizi.
6. Popo mbili zavuka mto – Macho.
7. Kiatu changu hakiishi soli – Wayo.
8. Nyama nje ngozi ndani – Firigisi.
9. Mama nieleke – Kitanda.
10. Panda ngazi polepole – Sima.
11. Nyumba yangu haina mlango – Yai.
12. Rafiki yangu anatembea kwa tumbo – Nyoka.
13. Askari mlangoni – Kufuli.
14. Kipo lakini sikioni – Kisogo.
15. Huku ngo na kule ngo – Giza.
16. Hushindana wakifuatana – Magurudumu.
17. Nimpigapo mwanangu watu hucheza – Ngoma.
18. Hawa wanaingia hawa wanatoka – Nyuki.
19. Bak bandika bak bandua – Nyayo.
20. Wanangu watatu mmoja akiondoka wengine hawafanyi kazi – Mafiga.
21. Wanangu wafa mmoja mmoja kila siku – Kiberiti.
22. Namsikia tu lakini simwoni – Upepo.
23. Pambo lenye mawe meupe na mkeka mwekundu – Meno.
24. Hukopa lakini halipi – Mauti.
25. Anatengeneza chakula lakini hali – chungu.
26. Mzazi ana miguu lakini mzaliwa hanayo – Kuku na yai.
27. Jangwa langu latoka mvuke – Upara.
28. Janga laniandama usiku kucha – Kunguni.
29. Likienda hulia lakini likirudi halilii – debe.
30. Fupa la bikizee li nje – jino.
31. Anakukodolea macho lakini hakuoni – picha.
32. Anayekitengeneza hakitumii lakini anayekitumia hakioni – Jeneza.
33. Ala lakini hashibi – sindano / mauti / kifo.

**AKISAMI**

- $\frac{1}{2}$ ______ Nusu
- $\frac{1}{3}$ ______ Theluthi / thuluthi
- $\frac{1}{4}$ ______ Robo
- $\frac{1}{5}$ ______ Khumusi
- $\frac{1}{6}$ ______ Sudusi / sudusu
- $\frac{1}{7}$ ______ Subui
- $\frac{1}{8}$ ______ Thumni
- $\frac{1}{9}$ ______ Tusui
- $\frac{1}{10}$ ______ Ushuri
- $\frac{3}{4}$ ______ Robo tatu
- $\frac{2}{3}$ ______ Theluthi mbili
- $\frac{4}{5}$ ______ Humsi nne
- $\frac{3}{8}$ ______ Thumni tatu

**MSAMIATI WA BIASHARA**

1. Pato lipatikanalo baada ya kuondoa gharama – Faida / Tijara / Kivuno / Chumo / Ziada.
2. Ukosefu wa faida hali ya kupoteza mali katika biashara – Hasara.
3. Uuzaji wa kiasi kidogo kidogo – Muuzaji rejareja/ Mchuuzi.
4. Bei ambayo haipunguzwi – Bei / Rafi.
5. Kipimo ambacho hakipunguzwi – Kipimo rafi.
6. Bei isiyokubalika kisheria / haramu – Bei ya kuruka .
7. Ujumla wa mali yanayomilikiwa na mtu au nchi – Raslimali.
8. Mali yanayotumika kutengeneza vitu vingine kama pambo kwa nguo – Malighafi.
9. Utajiri kama madini , misitu maziwa , mito vinavyopatikana katika mazingira - maliasili.
10. Kutumia pesa /Mali ili kuzalisha fedha / mali zaidi(ili kupata faida) – Uwekezaji.
11. Raslimali k.v inayotumika kuzalisha mali – Kitega uchumi.
12. Wekezeji mtaji katika biashara – Ujasiri amali.
13. Mali ya kuanzisha biashara / kupanulia – Mtaji. (capital)
14. Ufichaji wa bidha ili bei yazo iruke – Ulanguzi.
15. Upigaji biashara kwa njia haramu / isiyo halali – Magendo.
16. Pesa zinazobaki baada ya kununua vitu – Masalio
17. Bidhaa zinazonunuliwa kutoka nchi za nje – Madhuhuri. (imports)
18. Bidhaa zinazouzwa nchi za nje – Mahuruji. (exports)
19. Kodi ya kuingiza vitu nchini / kuziuza / ada ya forodha – Ushuru.
20. Pesa zinazotolewa na serikali mbalimbali kujiendeleza – Ruzuku.

22. Wakala – Ajenti
23. Cheki / hundi – Hawala.
24. Aendaye kununua bidhaa au huduma – mteja.
25. Kiwango kinachotolewa kutoka bei iliyotangazwa – Turuhani/ Kipunguzo.
26. Ushirikiano wa watu wawili katika shughuli za kibiashara – Ubia (Patnership)
27. Hali ya kusababisha mali ya uma imilikiwe na watu binafsi – Ubinafsishaji.
28. Hali ya kuzuia mwingine kufanya biashara / kushindana katika biashara – Ukiritimba.
29. Duka kubwa ambapo wateja hujichukulia bidhaa kutoka rafuni – Duka kubwa.
30. Sehemu ya mtaji katika biashara – Hisa.

## MAENEO YA UTAWALA

(i) Kata ndogo – Huongozwa na naibu wa chifu.
(ii) Kata / lokesheni – Huongozwa na chifu.
(iii) Tarafa / divisheni – Huongozwa na mkuu wa taarafa.
(iv) Wilaya / mudiria – Huongozwa na mudiri / Mkuu wa wilaya.
(v) Mkoa – Huongozwa na mkuu wa mkoa.
(vi) Taifa – Huongozwa na rais.

## UHUSIANO WA WATU NA NCHI

- Katika nchi yoyote kila raia ana uhusiano na taifa.

(a) Anayeipenda nchi yake na yu tayari kuipigania – Mzalendo.
(b) Aichukiaye nchi yake hata kutoa siri zake kwa adui – Msaliti.
(c) Anayekimbia nchi yake kutokana na matatizo kama vita – Mkimbizi.
(d) Anayetoroka nchi yake labda kwa sababu ya kisiasa – mtoro.
(e) Anayetembea nchi yake ikwa madhumuni ya kujionea kustarehe – Mtalii.
(f) Anayepeleleza mambo ya nchi nyingine kisirisiri – Jasusi.
(g) Anayewakilisha nchi yake katika nchi nyingine – Balozi.
(h) Anayeihamia nchi nyingine na kufanya makao ya huko – Mlowezi / Setla.
(i) Anayeitawala nchi nyingine isiyo yake – Mkoloni / Mbeberu.
(j) Aliyezaliwa katika nchi fulani – Mzaliwa.
(k) Aliyezaliwa mahali fulani na akaendelea kukaa huko – Mwenyeji.
(l) Ambaye amejitolea kufanya kazi ya ulinzi – Mwanamgambo.
(m) Mwenyeji wa nchi fulani – Mwananchi.
(n) Anayetumiwa na kiongozi mwingine kwa manufaa ya kiongozi huyo – Kibaraka / Karagosi.
(o) Anayefuata mfano wa utawala wa mabavu – Fashisti / Dikteta.
(p) Asiyependa mabadiliko – Mhafidhina.
(q) Anayetangulia kuanzisha jambo - Mtakadamu.

## MAHAKAMANI

1. Hakimu/Jaji – Kuamua kesi / kutoa hukumu.
2. Mshtaki – Aliyeleta malalamiko mahakamani.
3. Mshtakiwa – Aliyedaiwa / Kufikiriwa ndiye mwenye kosa.
4. Shahidi – Anayetoa ushahidi, aliyeona / kusikia tukio husika.
5. Wakili – Anayemtetea mshtaki / mshtakiwa.
6. Kiongozi wa koti – Anayeomwongoza na kuelekeza mkondo wa kesi.
7. Karani wa koti – Anayeandika matukio kotini.
8. Mshukiwa – Anayedhaniwa kuwa amehusika katika uhalifu fulani.
9. Mahabusu – Aliyehukumiwa kifungo gerezani / Jelani.
10. Hakimu mkazi – Hakimu anayeshughulikia mahakama fulani.
11. Mkuu wa sheria - Mshauri mkuu wa serikali kuhusiana na mambo ya sheria.
12. Kiongozi wa mashtaka – Wakili wa kuendesha mashtaka mahakamani.
13. Mdai – Mlalamishi anayepigania haki yake kutoka kwa mdaiwa.
14. Mdaiwa – Mtu anayetakiwa alipe au aonyeshe kitu cha mwingine.
15. Mtuhumiwa – Mshukiwa aliyefikiriwa amefanya kosa.
16. Kesi ya jinai – Kesi iliyo na uzito mkubwa kama kesi ya mauji.
17. Kesi ya uhaini – Kesi kutokana na kupanga njama ya kupindua serikali.
18. Ithibati / Ekzibiti – Vitu vinavyowekwa / kuwekwa mahakamani kama ushahidi.
19. Ahirisha kesi – kutangaza kesi isikilizwe siku nyingine.
20. Hatia – Kosa linalostahili adhabu.
21. Daawa – Kesi dhidi ya mtu mmoja na mwingine.
22. Kuruka kesi – Kukataa kukabiliana na kesi.
23. Kukata kesi – Kutoa hukumu-kuamua kesi.
24. Kata rufani – Kuomba kesi isikilizwe upya.
25. Dhamana – Malipo yanayotolewa na mshtakiwa ili yasikilizwe upya.
26. Faini – Fedha iniyotozwa kama adhabu na mwenye hatia.
27. Kizimba – Sehemu katika koti anamokaa mshtakiwa , mshtaki / shahidi.
28. Hukumu – Uamuzi katika kesi.
29. Korokoro – Seli ya kuwafungia washukiwa katika kituo cha polisi.
30. Rumande – Sehemu maalum katika jela wanamowekwa mahabusu ambao kesi hazijakamilika.
31. Jela – Wanapofungwa mahabusu wanapotumikia kifungo chao.
32. Pingu / Vikuku – Vyuma vya duara vya kufungia wahalifu hususan mikononi.

## MSAMIATI WA JIKONI

- Jiko - Chombo cha kupika : linaweza kuwa la makaa, stima ,mvuke,gesi na jua.
- Seredani - Jiko la makaa

**MASWALI**

**Andika sentensi hizi kwa umoja**

1. Maduka yauzayo manukato yamefungwa.
2. Mashamba yao ni makubwa.
3. Magari ya majanadume hayo ni makubwa.
4. Meno haya yatang'olewa.
5. Mashoka yale yatanolewa.

**(iv) U - I**

- Huchukua viambishi ngeli "U"katika umoja na "I" katika wingi tunapotumia pamoja na vitenzi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mti | Miti |
| 2. Mlima | Milima |
| 3. Mguu | Miguu |
| 4. Mkarafuu | Mikarafuu |
| 5. Mwembe | Miembe |
| 6. Mfarakano | Mifarakano |
| 7. Mzigo | Mizigo |
| 8. Mparachichi | Miparachichi |
| 9. Mkorosho | Mikorosho |
| 10. Mlimau | Milimau |
| 11. Mhindi | Mihindi |
| 12. Mchakato | Michakato |
| 13. Msitu | Misitu |
| 14. Mtambo | Mitambo |

**MASWALI**

**Andika wingi wa sentensi hizi**

1. Maji yamo mtungini.
2. Mti uliokatwa utauzwa bei ghali.
3. Mumea ambao uling'olewa umekauka.
4. Mparachichi hautapandwa shambani.
5. Mkebe utakaopatikana utatupwa shimoni.

**(v) I – ZI**

- Nomino za ngeli hii zikitumiwa pamoja na vitenzi huchukua kiambishi "I" katika umoja na "ZI" katika wingi .
- Ingawa maneno katika ngeli hii majina hayana umoja wala wingi.

**Mifano:**

- Herufi
- Ngoma
- Nyasi
- Kalamu
- Alama
- Tai
- Kalamu
- Ndoo
- Taa
- Sahani
- Kofia
- Njia
- Nyundo
- Ngozi
- Sufuria
- Sabuni
- Saa
- Motokaa
- Ajali

**MASWALI**

**Kanusha sentensi zifuatazo**

1. Mimi naandika barua.
2. Mbavu zimevunjika.
3. Kucha zake zitakatwa leo.
4. Ndwele zilizowapata zitatibiwa.
5. Mwashi atatengeneza kuta ndefu.

**(vi) U – ZI**

- Viambishi katika ngeli hii pamoja na vitenzi huwa "U" katika umoja na "ZI" katika wingi

| **Umoja** | **Wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| • Ufagio | Fagio | • Ua | Nyua |
| • Ubia | Mbia | • Ubinda | Mbinda |
| • Waraka | Nyaraka | • Ulimi | Ndimi |
| • Uta | Nyuta | • Wembe | Nyembe |
| • Uwele | Ndwele | • Ufunguo | Funguo |
| • Ukucha | Kucha | • Wayo | Nyayo |
| • Uchango | Chango | • Ufa | Nyufa |
| • Utambi | Tambi | • Ubeleko | Mbeleko |
| • Ukuta | Kuta | • Ubavu | Mbavu |
| • Uzi | Nyuzi | • Ubao | Mbao |
| • Waya | Nyaya | • Ubawa | Mbawa |
| • Uteo | Teo | | |

**MASWALI**

**Andika sentensi ziifuatazo kwa umoja**

1. Nyaraka zilizoandikwa zitatumwa kesho.
2. Nyembe zao zimepotea.
3. Nyaya za sitima ziliibiwa wiki iliyopita.
4. Simba wana kucha ndefu.
5. Msipoziba nyufa mtajenga kuta.

**(vii) U – U**

- Nomino za ngeli hii huainishwa kwa matumizi ya kiambishi "U". Nyingi za nomino hizi huwa za DHAHANIA hazina wingi.

**Mifano:**

- Unga
- Mchanga
- Ugoro
- Udhia
- Uzembe
- Uroho
- Uvivu
- Uji
- Ujinga
- Uzee
- Uchawi
- Ujeuri
- Usafi
- Ujana

**(viii) YA - YA**

- Ngeli hii huwa na maneno ambayo hayana umoja wala wingi.Huchukua viambishi ngeli "YA" pamoja na vitenzi.

**Mifano:**

- Mafuta
- Maarifa
- Manukato
- Mazingira
- Mateso
- Mali
- Mate
- Maziwa
- Mapambazuko
- Mazingaombwe
- Maakuli
- Makao

**(ix) KU – KU**

- Hii ni ngeli ya vitenzi.Huchukua viambishi ngeli "KU". Nomino hazina umoja wala wingi. Kukanusha kwa vitenzi ku huchukua 'to' k.m kutosoma

**Mifano:**

- Kusoma
- Kulia
- Kuimba
- Kula
- Kulima
- Kufa

- Kuiba
- Kuomba
- Kulala
- Kuandika

**Mifano ya sentensi**

(a) Kufa kwake hakukufurahisha wengi.
(b) Kusoma kwa James hakupendezi.
(c) Kuimba kwa Caleb kunapendeza.

**(x) PA - PA**

- Hutumiwa kuonyesha mahali maalum k.m
  - Pahali hapa
  - Pahali hapo
  - Pahali pale

**Mifano ya sentensi:**

(a) Pahali hapa ni pachafu
(b) Pahali pake pamechafuliwa

**(xi) MU - MU**

- Hutumika kuonyeshea undani wa mahali fulani k.m
  - Mahali humu
  - Mahali humo
  - Mahali mle

**Mifano ya sentensi:**

(a) Humo ndimo walimopatikana wezi.
(b) Humu nyumbani ndimo mnamokaa watu wengine.

**(xii) KU**

- Hutumiwa kuonyesha mahali kusikodhihirika k.m

(a) Mahali huku kunapendeza.
(b) Mahali huko ndiko alikopatikana.
(c) Mahali kule kuna nyoka wenye sumu kali.
(d) Kule ndiko kwao.
(e) Huku ndiko kulikofichwa silaha hatari.

**UUNDAJI WA NOMINO / MANENO**

- Tunapounda maneno mapya huwa tunakuza lugha ya kiswahili.

A. Kuunda nomino kutokana na vitenzi k.m

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| Lima | mkulima / kilimo / ukulima |
| Kata | mkato / mkataji / ukataji |
| Rithi | mrithi / mirathi / urithi |
| Imba | mwimbaji / wimbo / uimbaji |
| Soma | msomaji / usomi/msomi/somo |
| Linda | ulinzi / mlinzi / ulindaji |
| Pika | upishi / mpishi |
| Kaa | mkazi / ukazi |
| Vua | mvuvi / uvuvi |
| Cheza | mchezo/uchezaji / mchezaji |
| Sema | msemo / msemaji |
| Tibu | tabibu / matibabu / tiba |
| Lea | mlezi / ulezi |
| Jenga | ujenzi / mjengo / jengo |

B. Kuunda vitenzi kutokana na nomino k.m

| Nomino | | Kitenzi |
|---|---|---|
| Safari | - | Safiri |
| Utiifu | - | Tii |
| Mlo | - | Kula |
| Mkwezi | - | Kwea |
| Mfinyanzi | - | Finyanga |
| Ratiba | - | Ratibu |
| Kilema | - | Lemaa |
| Mshtuko | - | Shtuka |
| Sala | - | Sali |
| Maandalizi | - | Andaa |
| Athari | - | Athiri |
| Kifo | - | Fisha |
| Shibe | - | Shiba |
| Kicheko | - | Cheka |
| Usasi | - | Saka |
| Faraja | - | Fariji |
| Ibada | - | Abudu |
| Imani | - | Amini |
| Rehema | - | Rehemu |
| Ujuzi | - | Jua |
| Anasa | - | Anisi |
| Maelezo | - | Eleza |
| Mkongwe | - | Konga |
| Mbio | - | Kimbia |
| Mtukufu | - | Tukuza |

C. Kuunda nomino kutokana na sifa.

| Sifa | Nomino |
|---|---|
| Zuri | Uzuri |
| Erevu | Werevu |
| Vivu | Uvivu |
| Tundu | Utundu |
| Eusi | Weusi |
| Refu | Urefu |

D. Kuunda sifa kutokana na vitenzi.

| Kitenzi | | Sifa |
|---|---|---|
| Ogopa | - | Ogofya |
| Ona | - | Onevu |
| Ota | - | Otevu |
| Ongoa | - | Ongovu |
| Sikia | - | Sikivu |
| Tulia | - | Tulivu |
| Dhulumu | - | Dhalimu |

E. Kuunda majina kutokana na utendakazi.

| | |
|---|---|
| Kifutio | Chombo cha kufutia |
| Kinasa + sauti | Chombo cha kunasa sauti |
| Kipaza + sauti | Chombo cha kupasa sauti |
| Simutamba | Simu inayobebwa mfukoni, mkononi |

F. Taksiri kopo (utohozi)

- Huchukua maneno yasiyo ya Kiswahili na kuyafanya yawe ya Kiswahili kimatamshi na kimuundo k.m

- Leave - Livu
- Generator - Jenereta
- Fertilizer - Fataliza
- Operation - Operesheni
- Panel - Paneli

G. Akronimu

- Ni kufupisha maneno marefu / kuunga silabi ya mwanzo / baadhi ya silabi k.m

- Mafiga / mafya - Mawe matatu ya jiko la kuni.
- Uchaga - Sehemu ya kuwekea kuni.
- Dohani - Mfereji wa kutolea moshi jikoni.
- Susu - Chombo cha kuwekea sahani au chungu.
  Birika / buli - Chombo cha kutilia chai au kinywaji kingine.
- Kinu - Chombo cha kusagia nafaka viungo n.k
- Kikaango - Chombo cha kutumia kukaangia vyakula k.m chapati.
- Tanuri - Jiko la kuokea mikate.
- Jokofu / friji / jirafu - Chombo chenye mtambo wa kuleta baridi na kuhifadhi aghalabu vyakula.
- Degi - Sufuria kubwa ya kupikia chakula kingi.
- Sinia - Sahani kubwa ya mviringo hutumika kupakulia chakula.
- Mbuzi - Kifaa cha kukunia nazi.
- Kifumbu / kung'uto / kichujio - Kifaa cha miyaa cha kuchuja kinywaji.
- Chano / fua - Sinia kubwa ya ubao ya kupakulia chakula.
- Kihoro - Sahani ya mti
- Kata - Chombo cha kuchotea maji mtungini.
- Ungo / uteo - Kifaa kitumiwacho kupepeta vitu vya nafaka.
- Mwiku / kiporo / bariyo - Chakula kilicholala mpaka asubuhi.
- Ukoko - Mabaki / masazi yachakula yanayoganda kwenye chombo kilichopikia.
- Mashizi - Unga mweusi wa makaa. unaopatikana kwenye sufuria.
- Mlale - Utandabui mweusi utokanao na moshi jikoni.
- Kishuka / chamcha → Maakuli / chakula cha adhuhuri.

**VITENDO JIKONI**

- Kukoka moto - Asha moto.
- Kupuliza moto - Kusababisha moto. uwakekwa nguvu zaidi.
- Kuzima moto - Kupoesha moto.
- Kuteleka / kuinjika - Kuweka chungu au sufuria juu ya jiko.
- Kuepua / kuinjua - Kuondoa chungu au sufuria juu ya jiko.
- Kutokosa - Kuchemka
- Kutokota - Chemka kwa nguvu
- Pepeta - Rusharusha nafaka juu kuondoa makapi.
- Oka - Tia ndani ya tanuu la moto kitu kama vile mkate, keki, matofali ili kuivisha.

**VYOMBO KATIKA KARAKANA**

| Chombo | Matumizi | Anayetumia |
|---|---|---|
| 1. Utepe | Uzi wa kumia urefu | Seremala, mashonaji |
| 2. Mvuo/ mvukuto | Mfuko wa kutumia kupuliza moto | Mhunzi |
| 3. Nyundo | Kifaa cha kugongomelea | Seremala / mwashi |
| 4. Patasi/ chumasi/ jupa | Kutobolea mshimo kwenye mbao | Seremala |
| 5. Kekee | Chombo cha kutobolea mbao | Seremala |
| 6. Randa | Chombo cha kusawazisha mbao | Seremala |
| 7. Msasa | Karatasi ngumu ya kusawazisha mbao | Seremala |
| 8. Kipira | Randa ya kuviringa mbao | Seremala |
| 9. Maleti | Nyundo kubwa ya mbao | Seremala |
| 10. Msumeno | Chombo cha kukereza / kukata mbao | Seremala |
| 11. Bisibisi | Kutolea/ kuingiza misumari kukazia akrubi | Seremala |
| 12. Jiriwa | Kushikilia vitu imara vinapofanyiwa kazi | Seremala |
| 13. Ngubu | Kifaa cha kufanyia michoro | Seremala |
| 14. Mfuo | Kutobolea matundu | Seremala |
| 15. Mahati | Kupimia na kufanyia mistari | Seremala |
| 16. Cherehe | Kunolea vyombo | Mjumu/ Seremala/mpishi |
| 17. Jambeni | Msumeno mkubwa unaoshikwa na watu wawili | Mpasua mbao |
| 18. Maharazi | Shindano ya kushonea kiatu | Mshona kiatu |
| 19. Nguri | Nyundo ndogo ya mbao ya kutengenezea kiatu | Mshona kiatu |
| 20. Chenezo | Chombo cha kupimia urefu | Seremala/mwashi/mshonaji |
| 21. Pimamaji | Kupimia usawa au unyookaji wa kitu | Seremala/ mwashi |
| 22. Subana/tandoo/ kastabani | Kifaa cha kutumia kidoleni wakati wa kushona | Mshona nguo |
| 23. Kifusi | Udongo wa kujengea nyumba | Mwashi |
| 24. Kinoo | Jiwe la kutilia makali shoka, panga, makasi na kisu | |
| 25. Tezo | Kuchongea mbao | Seremala |
| 26. Sepetu/ koleo/ shepe | Kushikia vitu vinavyoundwa | Seremala/ mhunzi |
| 27. Fuawe | Chuma anachotumia mhunzi kuwekea chuma anachofua mhunzi. | Mhunzi |

**MAUMBILE YA NCHI**

- Mto – Bonde lenye maji yanayotiririka wakati wote.
- Ziwa – Sehemu yenye maji mengi ...zungukwa na nchi kavu.
- Bahari – Eneo kubwa la maji ya chumvi linalozungukwa na nchi kavu.
- Upwa – Sehemu ya pwani ambayo maji hujaa na hupwaa.
- Delta – Sehemu ya mto unapojigawanya

vipande viwili au zaidi unapoingia baharini.

- Kinamasi – Mahali penye tope au telezi.
- Chemichemi – Mahali maji yanapobubujika.
- Gema/genge/korongo – Mteremko mkali wa kwenye kingo za mto.
- Kisiwa – Eneo la nchi kavu lililozungukwa na maji.
- Msitu – Eneo kubwa lililo na miti mingi.
- Nyika – Sehemu inayoota nyasi na miti midogo.
- Jangwa – Eneo kubwa na kame ambalo kwa kawaida huwa na mchanga lisiloota nyasi wala miti.
- Tambarare – Nchi isiyokuwa na miinuko wala mabonde.
- Bonde – Sehemu ya ardhi iliyo katikati ya vilima viwili.
- Nguu / kilele – Sehemu ya juu kabisa ya mlima.
- Volkano – Mlipuko mkali wa moto inayotokea ndani ya dunia zaha ambayo mara nyingi husababisha milima katika uso wa dunia.
- Kreta – Sehemu inayopatikana juu ya mlima.
- Oasisi – Kisima cha jangwani.
- Kisiwa – Eneo la nchi kavu lililozungukwa na maji.
- Wangwa – Sehemu ya pwani iliyo na mikoko ambapo maji hujaa na kupwa.
- Ghuba – Sehemu kubwa ya bahari iliyoingia ndani ya pwani.
- Mgodi – Mahali palipochimbuliwa madini.
- Kituka – Mahali penye miti mifupimifupi iliyoshonana na nyasi.
- Jabali – Mwamba mkubwa.

## MSAMIATI WA HOSPITALI

- Hospitali ni mahali pa kutibia wangojwa au wawele. Hospitali ndogo huitwa dispensari / zahanati.

## SEHEMU ZA HOSPITALI

(i) Pambajio – Sehemu ya kuwapokelea wagonjwa.
(ii) Wodi – Sehemu ya kuwalaza wagonjwa wanaoendelea kupokea matibabu.
(iii) Kungawi – Chumba cha kujifungulia wajawazito.
(iv) Chumba cha upasuaji – Chumba cha kufanyiwa upasuaji wa wagonjwa.
(v) Wodi ya matibabu maalum – Chumba cha kushughilikia maradhi ambayo si ya kawaida.
(vi) Chumba cha matibabu ya kina – Chumba cha kiwango cha matibabu ya juu sana (i.c.u). Hususan kwa walio hali mahututi.
(vii) Chumba cha matibabu ya dharura – Chumba cha kuwatibia wale wanaohitaji matibabu ya haraka sana k.m wahasiriwa wa ajali.
(viii) Maabara – Chumba cha kufanyiwa utafiti.
(ix) Chumba cha dawa – Chumba cha kuhifadhia dawa zitolewazo kwa wagonjwa.
(x) Ufuoni / makafani – Mahali pa kuhifadhia maiti.

## VYOMBO MBALIMBALI HOSPITALINI

1. Eksrei / uyoka – Mashine ya kuonea viungo ndani ya mwili.
2. Machela – Kitanda cha kubebea wagonjwa.
3. Mikroskopu / hadubini – Kifaa kitumiwacho kuangalia vitu vidogo.
4. Dipriza – Chombo cha kuhifadhia baadhi za dawa.
5. Glovu
6. Bendeji
7. Plasta
8. Koleo

## WAFANYIKAZI HOSPITALINI

1. Daktari/tabibu – Anayetibu wagonjwa.
2. Muuguzi / nesi – Anayemsaidia daktari kuwatibu wagonjwa.
3. Mkunga_-_Anayesaidia wajawazito kujifungua
4. Mhazigi – Anayeshughulikia waliovunjika viungo.

## VITATE / VITATAMSHI

- Vitate ni maneno yanayotatanisha kimatamshi. Kwa vile kuna makabila na lahaja nyingi za lugha, kuna mkanganyo wa baadhi ya matamshi k.m s, sh, z
  - l, r
  - k, g
  - d, dh, t ,th
  - ch, j
  - n ng ng',m, mb na kadhalika

### Mifano ya vitate

- Kali---kitu ambacho ni chungu mdomoni.
- Ghali ----bei iliyo juu sana.
- Mahari-----malipo ya kuolea.
- mahali------maskani / pahali
- Fahari------majivuno / utukufu
- Ndoa--------nakahi / arusi
- Doa---------kasoro / alama
- Nchi--------taifa / jamhuri
- Inchi-------kipimo cha urefu
- Ama-------au pengine
- Hama-----kuhajiri / toka mahali
- Vuta------sukuma upate wako
- Futa------pangusa
- Asi--------goma
- Hasi------kumfanya ngombe dume maksai.
- Zamani---kale
- Samani---fanicha
- Kura------uchaguzi
- Kula------kubugia mlo
- Randa----zurura
- Landa----fanana
- Mchuzi----rojorojo inayotokana
- Mchuuzi---mwuzaji rejareja
- Mbali-----kinyume cha karibu
- Bali--------ila / lakini
- Yamkini---labda / pengine
- Yakini------hakika / kweli

- Masaibu—maafa / matatizo
- Masahibu—marafiki / wendani
- Kataa-------goma
- Kata----------kutema
- Bawabu-----mlinzi mlangoni
- Bawaba-----kipande cha chuma kwenye mlango.
- Njaa----------hali ya kutokula chochote.
- Jaa----------biwi la takataka / hali ya kuwa nyingi.
- Ungua------kuteketea
- Ugua--------hali ya kuwa mgonjwa.
- Bibi-----------nyanya
- Pipi----------peremende
- Karamu-----sherehe
- Kalamu-----kifaa cha kuandikia.
- Hapa--------mahali
- Haba---------chache
- Jongoo-----mnyama anayetambaa asiyeona.
- Jogoo-------kuku wa kiume
- Kipofu-------asiyeona
- Kibofu-------mfuko wa mkojo
- Kibovu------kilichooza / haribika
- Kipovu------maji ya sabuni

**SENTENSI ZENYE VITANZA NDIMI VITOKANAVYO NA VITATE**

1. Mkongwe aliyekonga na kukongoka alijikonga kwa mkongojo.
2. Nilikomea papo hapo komekome kama koko wa kome.
3. Si sudi si sada Sudi na Sada kunywa soda ya softa sokoni Sokomoko.
4. Cha mkufuu mwanafuu ha akila hu lakini mwanafuu mkufuu hu akila ha.
5. Mate wa Mwatate amtemea mate na kumkemea Mate wa Materi Mateni.
6. Chura shupavu alishtuka alipoharibu shura katika hupi iliyojaa chupi fupifupi.
7. Mchuuzi mwenye ujuzi wa uchuuzi alichuuza mchuzi wa mjusi juzi.
8. Karua na Kalua wararua kula za Rukia wa Karura Kuria.
9. Chacha ana shaka ya kuchacha kwenye chakacha baada ya kushuka kutoka Chuka.
10. Chukua mshumaa uwashe chumbani kisha ufiche chombo chake shaka chumbani.

**ZOEZI**

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa vitate vifaavyo.**

1. _____mwenye ______, ______kinachotoa _____ amepelekwa hospitali (povo,kibofu,kipofu, kibovu)
2. Joy alinunua _______ kihsa akaenda kwenye _______ (karamu, kalamu)
3. Baada ya kupiga _______ alienda ______(kula, kura)

**VISAWE**

Visawe ni maneno tofauti yenye maana sawa.

**MIFANO**

- Baraste - barabara / tariki.
- Taadhima - heshima / adabu / tasfida.
- Msichana - banati / binti / mwari.
- Ndoa - nikahi / arusi.
- Stadi - bingwa / farsi / ngwiji / mtaalam.
- Hamaki - kasirika / ghadhabika.
- Duni - dhalili / hafifu / nyonge.
- Ugali - sima / mbondo.
- Uliza - saili / hoji.
- Rika - umri / hirimu.
- Aibu - haya / tahayuri / soni.
- Simanzi - majonzi / jitimai / ukiwa / huzuni.
- Baradhuli—zuzu / zuge / bwege / juha / fala / mpumbavu / jinga.
- Hongo - rushwa / mlungura / kadhongo / chichimiri / chai.
- Afya - siha / zihi / rai / nishati.
- Kasoro - hitilafu / walakini / doa / taksiri.
- Ukuta - kiambaza.
- Mwizi - pwagu / mdokozi.
- Mnyama - hayawani.
- Mvulana - ghulamu / barobaro.
- Rafiki - sahibu / mwendani / msiri / swahiba / msena / azizi / muhibu.
- Maskini - fukara / fakiri / mlalahoi / mchochole / mkata / mtule.
- Tajir - mkwasi / kikore / lodi / mlalahai / bwanyenye.
- Macho – maninga
- Mwalimu - mdarisi / mkufunzi.
- Wasiwasi - dukuduku / kimeme /wahaka / wayowayo / hatihati / kiherehere kimuyemuye / kiwewe.
- Polepole - asteaste / taratibu / alaala.
- Kilimo – zaraa
- Lengo - nia / azma / tarajio / matilaba / dhamira.
- Chakula - mlo / maakuli.
- Ndoto - ruiya / njozi.
- Halati - hale / mbiomba /amati.
- Kazi - gange / amali /shughuli.
- Soko - chete / gulio.
- Binadamu - mahuluki / insi / mja / adinasi.
- Fujo - rabsha / rangaito / sokomoko / tendaberua /vurugu / vurumai.
- Samaki - nswi /swi
- Nguruwe – hanziri
- Tele - mzomzo / belele / sufufu / maridhawa / lufufu / kochocho.
- Mwisho - tamati / upeo / hatima / kilele.
- Mwendawazimu - afkani / punguani / chakaramu / zingwizingwi / mwehu.
- Adui - hasidi / hasimu
- Pesa - ngwenje / gome / fulusi / ghawazi /njenje.
- Ugonjwa - maradhi / ndwele.
- Wakati – abra / fursa.

**VITAWE**

- Vitawe ni maneno yenye maana zaidi ya moja k.m

**Meza:**
- kupitisha chakula kooni
- kifaa cha kuandaa meza

Vua:
- toa samaki majini
- toa nguo mwilini
- oka kutoka hatarini

Tembo: pombe
- ndovu

Nyanya: tunda la mnyanya
- bibi

Jaa:
- kufurika
- mahali pa kutupia takataka

Chungu: kifaa cha mfinyanzi
- aina ya wadudu
- kwa wingi
- kuwa na maumivu

Paa:
- aina ya mnyama kama mbuzi
- ruka angani
- zana ya mziki ipulizwayo

**ZOEZI**

Toa maana nyingine ya maneno yafuatayo.

- Panga
- Kata
- Ota
- Paka
- Kaa
- Buibui
- Mbuzi
- Mto
- Taa
- Kima
- Mbuni
- Kanda
- Ganda
- Tai
- Baa
- Mkungani
- Barabara

**METHALI**

- Methali hutumika kutufunza, kutuonya, kutushauri, kutuhimiza na kutuelimisha.

**Methali zinazotuhimiza kuwa na bidii:**

1. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
2. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.
3. Atangaye sana na jua hujua.
4. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
5. Mchumia juani hulia kivulini.

**Methali zinazotuhimiza kuwa na uvumilivu**

1. Mvumilivu hula mbivu.
2. Mwenye pupa hadiriki kula tamu.
3. Penye nia pana njia.
4. Penye mawimbi na milango ipapo.
5. Baada ya dhiki faraja.
6. Zito hufuatwa na jepesi.

**Methali zinazotuonya kuhusu tamaa**

1. Mtaka yote hukosa yote.
2. Tamaa mbele mauti nyuma.
3. Njia mbili ilimshinda fisi.
4. Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
5. Tamaa ilimwua fisi.
6. Mla kwa mawili hana mwisho mwema.

**Methali zinazotuonya kutodanganywa na uzuri wa nje**

1. Yote yang'aayo si dhahabu.
2. Vyote viowevu si maji.
3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.
4. Uzuri wa kuyu ndani mabuu.
5. Penye urembo ndipo penye urimbo.
6. Mdharau mwiba huota tende.

**Methali zinazotushauri kuyashughulikia mambo mapema**

1. Udongo uwahi ungali maji.
2. Kambale mkunje angali mbichi.
3. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
4. Chuma kiwahi kingali moto.
5. Samaki mkunje angali mbichi.
6. Moto uzime ungali cheche.

**Methali zinazotuliwaza na kutuonyesha uwezo wake Mola**

1. Kalamu ya Mungu haikosi.
2. Mungu hamsahau mja wake.
3. Liandikwalo ndilo liwalo.
4. Jitihada haiondoi kudura.

**Methali zinazotuhimiza kutenda mema**

1. Kwendako mema hurudi mema.
2. Tenda mema uende zako.
3. Wema hauozi.
4. Kumpa mwezio si kutupa.
5. Akataaye wengi ni mchawi.
6. Jina jema hung'aa gizani.

**Methali zinazotuonya kutotumainia jambo kabla litimie**

1. Kutangulia si kufika.
2. Kuchumbia si kuoa.
3. Kulenga si kufuma.
4. Usikate kanzu kabla mwana kuzaliwa.
5. Usihesabu vifaranga kabla hawachaanguliuwa.

**Methali zinazotuonya kutotegemea usaidizi wa mbali**

1. Kamba ya mbali haifungi kuni.
2. Fimbo ya mbali haiui nyoka.
3. Ulingo wa kwae haulindi manda.
4. Amadi kibindoni silaha iliyo mkononi.
5. Sanda ya mbali haiziki maiti.

**METHALI ZAIDI –Jaribu kutafuta maana ya ndani**

1. Zungua la mtukutu na mkaidi ni ufito.
2. Vumbi la kisonzo si la ufukwe.
3. Aliyefiwa huachiwa mengi.
4. Maisha ni mtego ukisepetuka umenaswa
5. Uso mrembo hauitaji mapambo.
6. Matendo hukidhi haja.
7. Mtu akitaka kuruka huagana na nyonga.
8. Hakuna nyongesa mbaya.
9. Mbwa hafi maji akiona ufuko.
10. Malipo ni duniani chendacho ahera ni hesabu.
11. Mchezea mavi hayaachi kumunukia.
12. Hakuna mchele usiokosa ndume.
13. Mzoea vya udalali vya kuchinja haviwezi.
14. Mtego bila chano haunasi.
15. Ulingo wa kwae haulindi manda.
16. Jino liking'oka ukubwani halioti ng'o.
17. Amezaye tonge kaamini koo lake.
18. Ajitengaye na maovu haingii hatiani.
19. Mtu hana kabila.
20. Raha ikizidi sana huwa karaha.
21. Hakuna kizuri kitokacho pazuri.
22. Mwenye kovu usidhani kapoa.

23. Mwana ni anga la nyumba.
24. Mkataa pema pabaya panamwita.
25. Njaa ni mwana malegeza na shibe ni mwana malevya.
26. Usikaange mbuyu ukawaachie wenye meno kutafuna.
27. Hakuna dhiki ya mtu mmoja.
28. Kusema dhahabu kujibu fedha.
29. Mkata hana kinyongo wala mwiko.
30. Kesi ya mungu haina wakili wala kukata rufani.
31. Kichango ni kuchangizana.
32. Uzee si ndwele wala lelemaa.
33. Kaa akiinua gando mambo yamekatika.
34. Mwana msikivu hakanywi mchana kutwa.
35. Mumunye huharibikia ukubwani.
36. Mnywa maji konzi moja kiu yake ipale pale.
37. Mzigo wa mlo haulemei.
38. Hakuna dhiki ya mtu mmoja.
39. Ndege mwigo hana mazoea.
40. Mapenzi ni kama mti huota popote.
41. Tumbo la mja halina kina chake.
42. Sumu haijaribiwi kwa kuonja.
43. Panapo utamu wa maisha pana uchungu wake.
44. Jino la pembe halinyimwi mcheshi.
45. Mla kunde hunya kunde.
46. Kiburi cha mende huishia motoni.
47. Mkwanju muwi una tumbiriwe.
48. Farasi hamuwawezi ndovu mtawalishani?
49. Enda na uchao usiende na uchwao.
50. Mtaka nyingi nasaba hupata nyingi msiba.
51. Mwana wa yungi hulewa senze.
52. Maji ya mbande ni mafu.
53. Usione ngiri analia ukadhani anacheka.
54. Kiendacho mavani hakina marejeo.
55. Ukubwa wa pua si wingi wa makamasi.
56. Ukubwa wa tumbo si wingi wa njaa.
57. Usishindwe na kupika ukasingizia jiko .
58. Ukitaka ua la waridi sharti udhurike.

## MSAMIATI WA MAKAO

1. Makao ya wavulana waliotiwa jando ni - Kumbi
2. Raisi huishi kwenye - Ikulu
3. Mfalme huishi kwenye - Kasri
4. Mtawala huishi kwenye - Kitala
5. Mfungwa hukaa kwenye - Gerezani / husuni
6. Makao ya mtu angojeaye kesi ikatwe - Rumande
7. Ng'ombe huishi kwenye - Zizi / chaa / zeriba / buruji
8. Samaki huishi kwenye - Majini
9. Kasuku huishi kwenye - Tundu
10. Kuku huishi kwenye - Kizimba
11. Fuko huishi kwenye - Shimo
12. Nyuni huishi kwenye - Kiota
13. Makao ya kiwavi - Kifukofuko
14. Makao ya panzi - Nyasini
15. Konokono huishi kwenye - Koa / kombe
16. Funza huishi kwenye - Vidoleni
17. Mchwa huishi katika - Kingulima / kishirazi / kichuguu / kidurusi
18. Jana huishi kwenye - Masegasega
19. Nyuki huishi kwenye - Mzinga
20. Buibui huishi kwenye - Utandabui / utando
21. Makao ya uchango - Utumbo
22. Mahali palipotengwa kuzikia watu - Makaburini
23. Nyumba ya waislamu - Msikitini
24. Chumba cha kupokelea wageni - Sebule
25. Anapotagia kuku - Choto
26. Panapoegeshwa magari - Maegesho
27. Mahali anaposimama mshitakiwa - Kizimbani
28. Mahali pa kupatiwa matibabu madogomadogo - Zahanati
29. Mahali wanapotahiriwa watoto wa kiume - Jandoni
30. Wanapojificha wanajeshi kwa ajili ya vita - Handaki
31. Mahali katika shule wanapolala wanafunzi - Bweni
32. Mahali palipohamwa - Mahame
33. Mahali wanapoogeshwa wanyama ili kuua kupe - Josho / dipu
34. Anaposimama imamu - Mimbari
35. Kituo cha kupumzika katika safari - Kambi
36. Bweni la wasichana - Dahalia
37. Mahali wachawi wanapofanya baraza zao za kisiri - Kilinge
38. Kiunga cha kupanda miti ya matunda / maua - Bustani
39. Nyumba ya kuwekea akiba ya chakula au vitu -Stoo / ghala
40. Fungu la nchi kavu lililozungukwa na maji pande zote - Kisiwa

## MSAMIATI WA MALIPO

1. Malipo apewayo mtu baada ya kustaafu - Kiinuamgongo
2. Malipo kwa mganga - Ada / kifunguamkopa / fungule
3. Malipo ya kujiunga na shule - Koto
4. Malipo unayolipa ili kumsomesha mtu - Karo
5. Malipo ya kuolea - Mahari
6. Malipo unayolipia nyumba isiyo yako ili uishi - Kodi
7. Malipo unayolipia bidhaa kutoka nje - Ushuru
8. Malipo ya mwisho wa mwezi - Mshahara
9. Malipo ya aliyeokota au kuokota kitu - Kiokozi
10. Zawadi ya ugunduzi wa kitu - Utotole / kiangaza macho.
11. Pesa anazopewa mtu kabla ya mshahara - Karadha / advansi
12. Malipo ya kumpa mtu aliye poteza mali / hasara / maumivu - Fidia
13. Malipo ya hiari kwa ajili ya kujenga taifa - Mchango
14. Malipo ya kwanza ya kumshika mtoto mchanga - Fola
15. Malipo anayopata mtu zaidi ya yale yake ya kawaida - Marupurupu
16. Malipo ya kuingilia mahali k.v michezoni -

Kiingilio
17. Malipo ya pesa za muda uliopita - Kasiraji
18. Malipo unayompa mtu uliyemwudhi ili kuondoa hasira zake - Mapoza / kombozi
19. Malipo kwa ajili ya kumtoa mtu damu - Arshi / dia.
20. Mali anayopewa mtu kutokana na mali ya marehemu - Urithi
21. Malopo ya kazi ya siku - Kibarua
22. Fungu la mtaji katika biashara ya ushirikiano - Hisa
23. Pesa anazotozwa kulipa mtu aliyekopesha - Deni
24. Kuweka kitu cha thamani kama dhamana - Rehani / rahani
25. Fedha inayotozwa kuwa ni adhabu kwa mwenye hatia - Faini / haka
26. Malipo ya kuonyesha shukrani kwa kutimiza ahadi fulani - Bahashishi
27. Malipo au fungu la nyama apokealo mchungaji - Uchinjio
28. Malipo apokeayo mvulana atokapo jandoni - Fichuo
29. Pesa za matumizi ya kila siku - Masurufu
30. Malipo ya mshukiwa yanayolipwa ili aachiliwe mahakamani ili kesi ifanywe baadaye - Dhamana
31. Malipo kwa ajili ya kupendelewa - Chai / kadhongo / hongo / mchirizi / mlungula.

## VIUNGANISHI

- Kiunganishi ni neno linalounganisha mafungu mawili au sentensi mbili kutoa mshikamano mzuri wa mawazo. Tuna aina ya viunganishi.

**(i) Viunganishi vya dhana ya kujumlisha.**

**Mifano:**

(a) Fauka ya - Fauka ya hayo, yeye ni mwenyekiti wa chama cha wafanyakazi.
(b) Licha ya - Alifanya mtihani licha ya kuwa mgonjwa.
(c) Isitoshe - Isitoshe tunafaa kutunza mazingira.
(d) Zaidi ya - Zaidi ya kufanya bidii alituzwa.
(e) Aidha / vilevile - Vilevile tunafaa kudumisha usafi.

**(ii) Viunganishi vipambanuzi vikatavu**

(a) Lakini - Alikuja lakini hatukuonana.
(b) Ila - Alienda kwao ila hakumpata mtu.
(c) Bali - Hakuja bali alimtuma mtoto wake.
(d) Ijapokuwa - Alijitahidi ijapokuwa hakufaúlu.
(e) Ingawa - Ingawa niliugua malaria nilifanya mtihani.

**(iii) Viunganishi vya dhana ya uchaguzi**

(a) Au - Niitie Omondi au Onyango.
(b) Ama - Nipikie wali ama sima.
(c) Wala - Hakuja wala kutuma mwakilishi.

**(iv) Viunganishi vya sababu**

(a) Kwa sababu:- Alifungwa kwa sababu ya wizi.
(b) Ili:- Alienda zahanarti ili atibiwe.
(c) Mradi:- Nitakukopesha pesa mradi uniahidi kuwa utanirudishia.
(d) Kwa ajili ya
(e) Mighairi
(f) Mintarafu
(g) Minajiri

**Viunganishi vilinganishi**

(a) Sembuse /seuze / fakaifa / kefu / kaifa:- Alimwua simba sembuse paka.
(b) Laiti:- Laiti ningejua nisingemkaribisha kwangu.
(c) Lau:- Lau utakuwapo nitakuja.

## VINYUME

- Vinyume ni hali nyingine ya kitu, mtu, hali, wakati, au tendo. Tuna vinyume aina:

**(i) Vinyume vya jinsia**

| Kiume - Kike | Kiume - Kike |
|---|---|
| Mwanaume – Mwanamke | Shahibu – Ajuza |
| Babu – Nyanya | Fahari – Mtamba/ mbarika |
| Bin – Binti | Ghulamu – Banati |
| Mtwana – Mjakazi | Beberu – Mbarika |
| Ami – Shangazi | Mtanashati – Mrembo |
| Jando – Unyago | Raisi – Mamataifa |
| Mjomba/ hau – Halati / hale | Mfalme – Malkia |
| Nyakanga/somo – Kungwi | Mwinyi - Nana |
| Pora – Tembe | Mjane – Mfaruku |
| Kapera – Mwanamwali | Bamkwe – Mamkwe |
| Jogoo/jiimbi – Koo/mtetea | Binamu – Bintiamu |
| Bavyaa – Mavyaa | Mgumba – Tasa |
| Rafiki – Shoga | |

**(ii) Vinyume vya tathmini /hali**

- Kibaya - Kizuri
- Tajiri - Maskini
- Safi - Chafu
- Polepole - Harakaharaka
- Mrefu - Mfupi
- Ukubwa - Udogo
- Mshenzi - Mstaarabu
- Faida - Hasara
- Mjinga - Mwerevu
- Mkali - Mpole

**(iii) Vinyume vya vitenzi hali ya kutendua**

- Pakią - Pakua
- Funika - Funua
- Funga - Fungua
- Shona - Shonoa
- Ezeka - Ezua
- Fumba - Fumbua
- Tega - Tegua
- Nuka - Nukia
- Waza - Wazua
- Inama - Inuka

**(iv) Vinyume vya vitenzi**

- Panda - Shuka
- Tii - Kaidi
- Ingia - Toka
- Bariki - Laani
- Uza - Nunua
- Enda - Rudi

- Vuna - Panda

**(v) Vinyume vya mwelekeo**

- Nje - Ndani
- Mwembamba - munene
- Shibe - Njaa
- Kutwa - Kucha
- Uhuru - Utumwa
- Sakafu - Dari
- Chini - Juu
- Ardhi - Mbingu


- Nyingi - Chache


**(vi) Vinyume vya vitenzi "KU"**


- Kuzaliwa - Kutozaliwa
- Kulia - Kutolia
- Kufa - Kutokufa
- Kuandika - Kutoandika
- Kucheza - Kutocheza
- Kuenda - Kutoenda
- Kusoma - Kutosoma
- Kulegea - Kutolegea


# TAJA MAUMBO HAYA



Mraba



Mstatili


Mchemraba



Msambamba sawa



Duara



Duaradufu



Mche duara



Kopa


Pembe tatu mraba



Pembe tatu


Pembe tatu pacha


Pembe tatu sawa


Tao


Hilali


Kashata/ Tiara